KUMBUKUMBU ZA MUNGU ZILIZOJARIBIWA NA WAKATI

Na kulimalizia tu hilo huku, kupitia Biblia, jinsi ambavyo sisi . . . mumekichukua Kitabu cha Ufunuo, na Kitabu cha Kutoka na cha Mwanzo. Na sasa nimekuja nyumbani kwenda kuwinda kuchakulo. Ni aminifu. Hamna lingine kwake, ni kuwa tu mwaminifu. Na, Ndugu Roy, unakwenda lini? [Ndugu Roy anasema, "Kesho."—Mh.] Kesho. Vema. Kwa hivyo tunapenda tu kwenda nyumbani wakati huu wa mwaka, kwa hiyo, ni, tunataka kupumzika.

2 Nimepoteza pauni ishirini tangu nilipowaona. Nilijipima kwenye mizani, nilipotoka kwenye mkutano huu, nilikuwa na uzito wa ratili mia moja sitini na tano; kisha nikarudi, nikawa na uzito wa ratili mia moja arobaini na tano. Kwa hivyo, ninajisikia kama nguo zangu zinaanguka. Kwa hivyo, nilipoteza uzito mwingi.

3 Na mama fulani, leo, nikitoka, dada mpendwa, alisema, "Ndugu Branham, omba kwamba niweze kuupoteza, pia."

4 Naye kidogo akiwa upande wa uzito, kwa hivyo nikamwambia, "Njoo tu, nenda mbele, hubiri kwa nguvu sana." Kwa hiyo, hayo ni karibu yote nijuayo, hakika itaupunguza. Lakini, hivi karibuni tutamaliza shida na majaribu.

5 Nilikuwa nikiwazia juu ya kuzeeka. Mwajua, miaka miwili zaidi, nitakuwa na hamsini. Whiu! Nakumbuka wakati Frankie Weber alipoweka. Amenipita umri kwa yapata miaka miwili tu. Aliweka robo kwa sadaka ya siku ya kuzaliwa kwake, hapa. Nami nikakonyeza jicho langu, nikawaza, "Jamani, Frankie Weber, umri wa miaka ishirini na mitano, robo ya mia!" Ni nusu sasa. Haichukui muda mrefu, sivyo? Inaendelea moja kwa moja tu.

6 Hatutakaa muda mrefu. Asubuhi ya leo tu, wakati ndugu yetu mpendwa alipokuwa akileta ujumbe huo wa ajabu sana, nina hakika sote tuliufurahia. Basi ilitokea niliwazia jambo fulani alipokuwa akihubiri, kule nyuma, nami nikawazia, "Labda huenda Bwana akanipa Andiko kwa ajili hiyo." Nilimfanya asome kidogo usiku wa leo kutoka kwenye Neno la Mungu lililobarikiwa. Na sasa mimi . . . dakika chache tu za kuzungumza, kisha tutawaombea wagonjwa, kama kawaida.

7 Na Jumatano usiku, Jumatano hii ijayo usiku, Bwana akiruhusu, ningependa kuanzia katika Kitabu cha Waebrania, kama ni sawa. Na Kitabu cha Waebrania, kwa ajili ya somo. Na halafu, labda, Jumapili asubuhi ama Jumapili usiku, tuendelee

mbele. Ndipo Jumatano ifuatayo usiku, labda tulichukue tena, tuendelee tu kulichunguza hilo pande zote, katika Maandiko.

8 Na kuna mambo kadhaa ambayo niliona kanisani, wakati tu nikipitia, ambayo nadhani yanapaswa kufundishwa kidogo, mnajua, mambo ambayo yanaonekana kudhoofisha kidogo. Nami nafikiri tungeweza kulichukulia pale katika Waebrania. Ni—ni mlango mzuri sana, mahali pazuri sana pa kusoma. Sasa, Ndugu Neville. . .Nilikuwa naenda. . .Hilo lilinijia akilini, nikishuka huku.

9 Nami nina Agano Jipya tu hapa, na ninasoma kutoka katika Biblia ya Collins, maandishi yake ni makubwa zaidi. Nimeninii. . .Baada ya kufikia karibu hamsini, sina budi kuisogeza mbali sana nami, ili kusoma maandishi hayo madogo sana; ni mwanga mbaya, hata hivyo. Nami ninatoka nje kwenye mwanga wa jua na bado ninaisoma. Lakini wakati mwanga unapopungua kidogo, inanilazimu kuisukumia mbali. Naye daktari aliniambia kwamba hivi karibuni nitakuwa na miwani ya kusomea.

Nami nikamuuliza, "Macho yangu yalikuwa na shida?"

10 Naye akayapima. Kasema, "Hapana. Kumi kwa kumi, hayo ni mazuri mno. Ishirini kwa ishirini ni kawaida, na—na kumi na tano kwa kumi na tano ni bora zaidi." Na kumi kwa kumi, ni, hayo tu ndiyo angeweza kuisoma. Kwa hiyo ningeweza kusoma popote alipotaka, kwa mbali. Aliweka kitu fulani nje, nami nikaanza kukisoma. Alipofika karibu zaidi, niliendelea kusoma polepole zaidi na zaidi. Nilisimama ilipofikia *hivi*. Akasema, "Loo, naam, umepita arobaini."

Nami nikasema, "Naam."

11 Akasema, "Vema, kwa kawaida, mboni za macho yako zinakuwa bapa." Kasema, "Sasa, kama ukiishi maisha mazuri, marefu, utapata macho yako ya pili, natumaini. Hapo ndipo unaweza kusoma tena."

12 Lakini, unajua, nilikuwa nikiwazia tu, hiyo haiko mbali sana, kwa jambo hilo. Muda kidogo tu. Ndugu Tony, hiyo ni mbaya, sivyo? [Ndugu Tony anasema, "Hapana."—Mh.] La, sivyo. Ni jambo la heri. Ninazeeka, kwa njia moja, na mchanga kwa nyingine, kwa sababu ninaenda kwenye ule mwili mchanga, usiopatikana na mauti, uliobarikiwa, ambako, ndugu, hakutakuwako na jambo baya Kule. Nami ninauishia tu wakati huo. Huo utakuwa ni wa ajabu.

13 Sasa, kabla sijasoma kifungu cha kumalizia, neno moja tu Kwake tunapoviinamisha vichwa vyetu.

14 Tunaamini, Mungu Mwenyezi, kwamba unakusudia watoto Wako wawe na furaha. Haikusudiwi sisi kukunja uso na kuhuzunika, kwa maana imeandikwa, ya kwamba, "Moyo wa furaha huchangamsha kama dawa." Nasi tunapenda kufurahia

baraka Zako na kuwa na ushirika huu mkuu wa pamoja. Na wakati sisi . . .

15 Kama waumini katika Neno Lako, tunashirikiana kwenye Neno. Hilo ndilo lililotuleta hapa, si kusikia tu Ujumbe, bali kuabudu na kushirikiana na Wewe, kwa kusoma na kuhubiri Neno. Sasa, Bwana, Wewe hutavunja matumaini yetu. Nina hakika Wewe utatubariki katika saa hizi.

16 Mbariki mchungaji wetu mtukufu na mwema, Bwana. Tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja naye. Na kama nilivyomwona leo, katika mahubiri yake, na kumwona akitabasamu alipoimba wimbo huo, "Hivi karibuni nitamalizana na shida na majaribu." Na wale kina dada, na jinsi walivyouimba huku kwenye viwanja vya miti na mikutano ya kambi. Na itakwisha, moja ya siku hizi, kisha twende kwenye Raha hiyo tukufu.

17 Sasa, Baba, tubariki tunaposoma Neno Lako, na tumelisoma, na kuburudisha nia zetu na mioyo yetu. Basi nena nasi, usiku wa leo. Na wakati ibada itakapokwisha, nasi tuanze kwenda nyumbani kwetu, jalia tuseme, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

18 Sasa pamoja na ujumbe mzuri sana kama huo wa kiinjilisti tuliokuwa nao asubuhi ya leo, basi nilikuwa nikiwazia, kwamba, mwajua, Ndugu Neville alikuwa akizungumza kuhusu kuwalisha watoto kupita kiasi. Ambalo, unaweza kufanya. Lakini sasa, usiku wa leo, tuna mazungumzo kidogo tu kwa ajili ya kanisa. Haya ni maongezi tu kwa ajili ya kanisa. Nami ningependa kusoma . . . sehemu nyingine ya Maandiko, katika Agano Jipya, Mathayo mlango wa 24, na kifungu cha 35, Yesu akizungumza.

> *Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*

19 Somo langu usiku wa leo ni ku—kumbukumbu: *Kumbukumbu Za Mungu Zilizojaribiwa Na Wakati.*

20 Na nina matangazo machache. Naamini niliyatangaza, kwa ajili ya . . . na wengine hapa ambao . . . kuhusu mkutano utakaoanza na Waebrania, mlango wa kwanza, Jumatano usiku, Bwana akipenda. Sababu inayonilazimu kuutaja, ni kwamba, kama vile, mikutano yangu, ninaweza kuwa mahali pamoja, Naye ataniita pengine. Inanibidi tu kwenda jinsi anavyoniita Yeye, mwajua.

21 Hiyo ndiyo sababu siwezi kuwa kama Ndugu Oral Roberts na jamaa hao ambao hupanga mikutano yao miaka miwili au mitatu mbele, na, "Tutakuwa huko," na hao wanaume wakubwa wakakamavu wa imani. Wao—wao—wao wana ujumbe wao.

22 Lakini Ujumbe wangu ni popote tu Mungu anapotuma, iwe ni hapa, pale, popote pale. Inanibidi niende wakati tu Yeye anaponituma. Na ni huduma mbili mbalimbali; ila, Mungu yeye yule, Mungu yeye yule hasa.

23 Nilikuwa nikiwazia, jana, katika mazungumzo yangu na mvulana jirani. Naye akasema, "Unajua, maskini mchungaji fulani," akasema, "ni mtu wa ajabu sana." Kasema, "Mimi na mke wangu tulikuwa tumeketi tumevaa pajama zetu," kisha kasema, "yapata saa tano usiku, ndipo akaja na kubisha mlangoni. Kasema, 'Nimepitia tu hapa kunywa kikombe cha kahawa pamoja nanyi.'" Mnaona? Halafu akasema, "Alivuka mtaani hadi kwa jirani mwingine, nao walikuwa karibu kwenda kulala, naye akala biskuti kule. Na ninii tu . . . " Kisha akasema, "Ame—amekuwa na shule ndogo ya Biblia kwa ajili ya watoto wadogo, naye alikuwa na watoto wengi sana kule, yeye pamoja na mkewe, mpaka wakalazimika kupiga hema huko nje, wapate kuwahudumia watoto."

24 Ndipo nikarudi, nikaanza kuwazia, "Unajua, hiyo ni kweli. Huyo, huyo ni—huyo ni maskini jamaa wa ajabu." Nami naamini, Ndugu Fleeman hapa, ninaamini mvulana wake huenda kwenye Kanisa la Kilutheri la Imani hapa juu, maskini mtu mzuri sana pamoja na mkewe, wanafanya kazi kubwa kwa Bwana. Ndipo nikawazia . . . Nikaanza kuosha gari langu, na—nami nikavunjika moyo. Nikawazia, "Ni kwa nini siwezi kufanya hivyo, mnaona, kuzunguka, niwakusanye watoto wote, wanifuate kote? Nawapenda watoto. Basi ni kwa nini siwezi kuruka nyumba kwa nyumba, huku na huku, namna hiyo?"

25 Ndipo kitu Fulani kikaniambia tu, "Hukuitiwa hilo. Anafanya tu yale Mungu aliyomwambia."

26 Lakini hatuna budi kuwa na mtu fulani atakayesimama hapa nje, kama akina Oral Roberts na hao wengine, Yoshua na upanga, pamoja na Ujumbe wa imani na ukombozi. Basi, mnaona, hatuna budi kuwa na wale wanaoweza kuwa na . . . wa namna hiyo, na mtu anaweza kuwa na *hiki,* lakini yote yanaenda pamoja kutengeneza kitengo kimoja kikubwa. Hilo ni Kanisa la Mungu.

27 Nikizungumza muda mfupi uliopita na msichana mmoja, aliyekata tamaa na kuvunjika moyo. Nami nilikuwa nikijaribu kumwambia jinsi ambavyo—ambavyo mwanamke na mwanamume hawajatengana, wao ni mtu yule yule. Mtu alifanya . . . Mungu alimwumba mtu, mume na mke pia; alikuwa mtu. Hiyo ni kweli. Ndipo akawatenganisha katika mwili na kuwafanya tofauti, bali akawaunganisha pamoja kuwalea watoto wao, kama kitu kimoja. Na hivyo mwanamume, mkakamavu na tabia zile zile, naye mwanamke ni se—se—sehemu ya upendo ya mwanamume. Kwa hiyo, wako pamoja. Hiyo ni . . . Mungu aliwatenganisha. Lakini wote wawili

walikuwa mtu yule yule, m-w-a-n-a-m-u-m-e. Naye mwanamke anaitwa mwana-mke, hiyo ni kweli, maana alitwaliwa kutoka kwa mwanamume. Yeye ni sehemu ya mwanamume. Lakini ma—maishani hapa, katika mwili, walitenganishwa. Katika roho, wao ni kitu kimoja.

28 Nami nilikuwa nikizungumza kuhusu wanaume kupoteza upendo wao kwa mke wao, wala hawawapendi kama walivyofanya walipokuwa wapenzi. Aibu kwenu. Mnapaswa kuwapenda. Yeye sikuzote ni kipenzi chako. Kabisa. Hiyo ndiyo sehemu anayopaswa kuwa. Nawe unapaswa kumtendea hivyo. Loo, kamwe usiache hiyo fungate ndogo ikome, maana haitaisha, Mbinguni. Mtakuwa mmoja kikamilifu, Kule. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo wote . . .

29 Vema, inaonekana kana kwamba baadhi ya wanawake walipaswa kusema "amina" kwa hilo. Kamwe—kamwe msinifanye nisikie, "Sikuzote unawakemea wanawake, na kuzungumza namna hiyo." Dada Hickerson, kwa nini hukusema kitu, ama mtu fulani kule nyuma, aseme . . .? Ulisema? [Dada Cox anasema, "Amina."—Mh.] Asante, Dada Cox. Hilo ni zuri sana. Ndugu Cox, hilo ni kwa ajili yako, popote ulipo sasa. Vema. Naam, bwana.

30 Wala hatupaswi kamwe kusahau kuheshimiana. Sikuzote iweni wapenzi. Kamwe msiache ukome.

31 Mvulana Mkatoliki alinijia, si muda mrefu uliopita. Mkewe alikuwa anajitenga. Akasema, "Billy, nachukia kuja kwako; mimi ni Mkatoliki, nawe Mprotestanti." Kasema, "Kasisi alinifukuza nyumbani kwangu, muda mfupi uliopita."

Nami nikasema, "Kwani kuna nini, Ham?"

32 Akasema, "Vema, akaniambia." Kasema, "Mimi hunywa kidogo," kisha kasema, "usiku, ninafanya kazi kwa bidii." Kasema, "Mke wangu anafikiri inanibidi kuja kila usiku na kumbusu, na kumkumbatia, na kufanya kana kwamba tulikuwa tukijiandaa kufunga ndoa." Kasema, "Tulioana na tukapata watoto kadhaa." Kisha kasema, "Sisi, huo ni wakati . . . "

33 Nikasema, "Masalale, ngoja kidogo, jamani. Umekosea. Umekosea. Hivyo ni sawasawa na ilivyokuwa kabla ya kufunga ndoa. Unaona? Inakupasa kukumbuka hilo sikuzote." Nikasema, "Ana umri wa miaka arobaini sasa, wakati ambapo anahitaji uangalizi wako kabisa."

34 Kwa hiyo, walikuwa na mahakama ya talaka. Naye akasema, "Sijui nitakalofanya."

35 Nikasema, "Nenda, ukamwite. Kama ningeenda kule, kama Mprotestanti, asingenipokea. Lakini mimi . . . Unaona?"

Kasema, "Loo, anakupenda."

36 Nami nikasema, "Hilo, nenda tu ukamwite, mwambie kwamba umebadilisha mawazo yako."

37 Na kwa hiyo kesho yake, nilikuwa nimempigia simu hakimu na kuzungumza naye. Nami nikamwambia mvulana huyu, nikasema, "Nitakuwa nimeketi papo hapo chini ya orofa ambapo hakimu atawakaripia. Nitakuwa nikiwaombea. Usimwambie mkeo kuhusu hilo."

"Vema."

38 Kwa hiyo, nilikuwa huko chini, nikiomba. Baada ya kitambo kidogo nikasikia mwaliko mdogo ukishuka chini kwenye vipandio, nao hawa hapa wakaja, wakiwa wamekumbatiana, wamejaa tu tabasamu, mwajua. Akasema . . . Nikasema, "Vema, aloo, hapo!"

39 Naye akasema, "Ndugu Branham, sijakuona kwa muda!" Naam, dakika thelathini, mnaona. "Muda tangu nilipokuona!"

40 Naye mke akasema, "Mbona, Kasisi Branham, sijakuona kwa muda mrefu! Nina furaha kukuona tena!"

41 Nikasema, "Asante. Mbona," nikasema, "mnaonekana kama mlikuwa vipenzi."

"Loo," akasema, "tunaendelea vizuri tu. Sivyo, mpenzi?"

Mke akasema, "Naam, tunapendana, mpendwa." Nami . . . Mke akasema, "Njoo ukatuone wakati fulani, Kasisi."

42 Nami nikasema, "Asanteni, sana." Nikasema, "Kwaherini, ninyi!" Wakapita, maskini yule jamaa akageuka na kupunga mkono tena, namna *hiyo*. Yote yalitokea. Hiyo ni kweli.

43 Upendo hushinda kila kitu. Hiyo ni kweli, u—upendo tu. Unaweza kuwa na ishara zako zote na vithibitisho, lakini nipe tu upendo. Hilo—hilo latosha, kwangu mimi. Loo, jamani!

> Mwana-Kondoo mpendwa anayekufa, Damu Yako ya thamani
> Kamwe haitapoteza nguvu zake,
> Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
> Litakapookolewa, lisitende dhambi tena. (Mnaona?)
>
> Tangu kwa imani nilipokiona kijito hicho
> Kilichosababishwa na vidonda vyako vinavyotiririsha,
> Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu,
> Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

Hiyo ni kweli. Loo, ajabu!

44 Sasa, kumbukumbu za wakati zilizojaribiwa! Ambapo nilipata wazo hili asubuhi ya leo, lilitokana na ujumbe wetu kwenye shule ya Jumapili, ujumbe wa kiinjilisti, ambapo ndugu yetu alizungumza juu ya Eliya. Ambapo alitaka . . . Wavulana hawa, zile shule za manabii, jinsi walivyotaka kujenga namna

fulani ya shule kubwa. Nalo likanijia akilini mwangu, nami nilikuwa nikiwazia juu ya mawazo ya "kumbukumbu."

45 Sasa, kumbukumbu ni ja—jambo kubwa. Tunazithamini kumbukumbu. Nao watu wengi, katika maisha haya, wamejaribu kuacha nyuma yao aina fulani ya kumbukumbu. Karibu watu wote wanapenda kufanya hivyo. Wanaweka makaburini mwao, alama kuu. Hiyo ni sawa. Hakika. Nathamini hilo. Hiyo ni—hiyo ni sawa. Halafu wengi wanajaribu kujenga madhabahu makubwa.

46 Kumbukumbu moja ambayo ningependa kuirejea sasa, iko Ohio, na kulikuwako na kafiri. Ninasahau jina lake. Ninayo hiyo picha mahali fulani huko kwenye vitabu vyangu nyumbani. Ambapo, aliupinga Ukristo kwa dhati sana, hata alitaka ajengewe kumbukumbu, baada ya kifo chake, huku mguu wake umeikanyaga Biblia, amenyoosha kidole namna *hiyo,* na kusema, "Ondoleeni mbali ushirikina wa kidini, mkaifuate sayansi ya kisasa." Basi alipokuwa akifa, alisema, "Endapo nimekuwa makosani, nyoka watatambaa kutoka kaburini mwangu." Naye alipokufa, walikuwa bado wanatupa mchanga kaburini nao wakawaua nyoka wakubwa wawili au watatu. Na leo, kwenye makaburi hayo, mhudumu mmoja alipiga picha hivi majuzi akaniletea na kunionyesha, na kuning'inia juu ya minyororo kwenye ploti yake . . . Hilo eneo la kaburi ni mahali pazuri, lakini kilima chake si kitu ila lundo la nyoka. Na haijalishi, hata katika msimu wa majani kupukutika na msimu wa baridi kali, nyoka bado hutambaa kutoka kaburini mwake. Kumbukumbu! Mungu anizuie nisiwe na kumbukumbu kama hiyo, wala yeyote wenu.

Kwa hivyo kuna kumbukumbu, hata hivyo, kumbukumbu kubwa.

47 Ninawazia juu ya Yoshua, yule shujaa hodari wa vita. Jinsi alivyokuwa mtu mashuhuri, ambaye alichukua silaha za Musa, kama kiongozi wa Wayahudi hawa milioni mbili. Musa akiwa mteule, aliyeitwa atoke, aliyetengwa kwa ajili ya huduma. Naye Yoshua, kuingia na kupachukua mahali pa mtu huyo, hakika lilikuwa ni jambo kuu kufanya, kutimiza wajibu wa nabii huyu. Shujaa mwenye nguvu, aliyeitwa, aliyechaguliwa tangu zamani na kuteuliwa na Mungu. Miaka mia nne kabla hajaja, Mungu alisema angewakomboa na angewazuru. Naye Musa alikuwa shujaa wa namna gani!

48 Hakuna mtu aliyepata kuchukua mahali pa Musa, kupatimiza, mpaka Yesu Kristo alipoweza kupachukua. Naye akasema, mwenyewe, "Bwana Mungu wenu atawaondokesheni Nabii miongoni mwenu, kama nilivyo mimi. Na itakuwa, kama hamtamsikia Nabii huyu, yeyote ambaye hatamsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali." Vema.

Sasa, kumbukumbu hii kuu.

49 Naye Yoshua alikuwa ameshuka mtoni. Na baada ya Musa kufa, Yoshua alipachukua mahali pake. Naye Mungu alikuwa pamoja na Yoshua. Naye akasema, "Sasa jitakaseni, zifueni nguo zenu, na mjitenge, wala msiwakaribie wake zenu. Ndipo siku ya tatu, Mungu atafanya jambo fulani." Loo, mimi . . .

50 Moja ya siku hizi usiku, ibada za Jumapili, ninataka kuhubiri juu ya hiyo "siku ya tatu," na kuwaonyesha ni nguvu gani zilizomo ndani yazo, hizo tatu. Nililitaja hilo asubuhi ya leo katika maombi, kila mtu alikuwa na mambo matatu katika nyumatiki za Biblia.

51 "Sasa, siku ya tatu mtauona utukufu wa Mungu." Sasa ilininii . . . ilionyesha kwamba alijua vyema kile alichokuwa anazungumzia, kwa sababu alitaja wakati hasa ambapo kilikuwa kinaenda kutukia. Nami naweza kuwazia jinsi Yoshua alivyojisikia, aliposimama pale mbele ya Waisraeli hao wote. Sasa, neno lake halina budi kuwa kweli. Na hiyo hapo Yordani iliyofurika.

52 Mnaona, tabia ya mtu inajulikana kwa matendo yake. Chochote ulicho, matendo yako yanathibitisha kile ulicho. Haijalishi ni kiasi gani unashuhudia, chochote unachosema, kwa ubaya au uzuri, hilo halina uhusiano wowote nalo. Matendo yako yanaonyesha kile ulicho, yanaonyesha kile ulicho ndani. Kila kazi unayofanya, inadhihirisha kile ulicho.

53 Na ninyi wafanyabiashara, kama mkifanya tu kazi ovyoovyo, mnaona ninachomaanisha, kazi nusu-nusu tu, msifanye hivyo. Ikiwa huwezi kuifanya kwa usahihi, usifanye kabisa. Hiyo ni kweli.

54 Unapomjia Kristo, ikiwa huwezi kabisa kujitolea, kwa hali na mali, na kumjia Kristo, usije kabisa. Lakini unapotaka kweli kuwa Mkristo, jitokeze. Lifanye halisi. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka uwe. Na hiyo ita—hiyo itathibitisha, matendo yako yatathibitisha tabia yako ilivyo. Tabia yako inajulikana kwa matendo unayofanya.

55 Naye Yoshua, sasa, neno lake lilikuwa hatarini; naam, bwana, kama—kama tu Nuhu wa kale. Lakini Yoshua hana budi kuvuka mto huu. Na ilionekana ni kama alichagua wakati mbaya sana ambao ungeweza kuwaziwa. Ilikuwa katika mwezi wa Aprili. Na huo ni wakati theluji inayeyuka huko Uyahudi, na kushuka kupitia milimani, nao maskini Yordani una matope, nao unaenea nje hata—hata makondeni, kuyanywesha mashamba ya Yordani. Basi ilionekana kama, iwapo ingekuwa ya hisabati, au—au ya kielimu, au ya kisayansi, a—alichagua wakati mbaya sana katika mwaka mzima kuvuka Yordani. Lakini Mungu anapenda kuchukua nyakati za namna hiyo kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu.

56 Nao watu wa Mungu, wanaomwamini Mungu na kujua kile ambacho Mungu ameahidi, hawaogopi kufanya hivyo, kwa

sababu Mungu atashikilia Neno Lake, hakika tu kama Yeye alivyo Mungu.

57 Ndipo aliposema, "Kwanza, chukueni sanduku mwendelee mbele." Na wakati miguu hiyo ya makuhani ilipougusa huo Yordani, haidhuru ulikuwa unavuma jinsi gani, na jinsi ulivyokuwa ukifurika, ulifungua njia kwa Neno la Milele la Mungu, kwa maana Neno lilikuwa ndani ya lile sanduku. Yesu alisema, sasa, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Kwa hiyo, Yoshua, akijua kwamba neno lake halina budi kutulia juu ya Neno la Mungu, basi alilitanguliza Neno la Mungu.

58 Laiti ninyi wagonjwa hapa usiku wa leo mngefanya hivyo, muweke Neno la Mungu pamoja na maungamo yenu. Wekeni maungamo yenu, yaaminini na kuyaweka huko nje; na kuviita vitu hivyo, ambavyo havipo, kana kwamba vilikuwapo. Ndipo tunaendelea vema. Fanyeni hivyo. Neno la Mungu litayatimiza.

59 Ndipo miguu ya makuhani ilipougusa Yordani, ulirudi tu nyuma, upande upande. Nayo maji yakazuiliwa.

60 Je, mnatambua? Kunguruma kwa mto huo kungalisababisha ufuko pale, katika muda wa dakika ishirini, ungekuwa mkubwa kama—kama baadhi ya mabwawa haya makubwa ya kisasa tuliyo nayo, na Bwawa la Jabali la Colorado huko nje. Jinsi Yordani unavyopitia huko kwa kasi, ukitoka milimani, kwa nguvu sana, nao unapita kasi kupitia yale mabonde.

61 Na wakati watu milioni mbili wanaotembea kwa miguu, pamoja na wanawake na watoto, ukubwa huko, labda ilichukua saa nne au tano, au zaidi. Nanyi mnaonaje? Mto huo ungejaa. Lakini, Mungu aliuzuilia huo mkondo. Amina. Loo, napenda hilo. Akaizuilia mito! Nayo yakatulia pale mpaka walipovuka.

62 Kisha Mungu akamwambia Yoshua, "Tunataka kufanya kumbukumbu ya jambo hili. Nenda huko ukamtume kila Mwisraeli, mmoja kutoka katika kila kabila, wakaokote mawe kumi na mawili na kufanya kumbukumbu. Nayo kumbukumbu hii itakuwa ya kwamba watoto wenu watakapopitia njia hii, watauliza, 'Ni kitu gani kilichosababisha mawe haya kuwa hapa?' Nanyi mtawasimulia jinsi Mungu alivyouzuilia Yordani." Hiyo ni kumbukumbu ya ajabu. Siku moja natumaini kuyatazama mawe hayo, hivi karibuni, ambapo bado yanasimama kama kumbukumbu. Lakini basi nawazia juu ya—ya kumbukumbu nyingine. . . Hiyo ilikuwa ni kumbukumbu iliyobarikiwa jinsi gani!

63 Ndipo ninawazia juu ya kumbukumbu nyingine, siku moja, wakati mwanamke fulani alipokuwa amefanya chaguo baya. Aliamua kutokaa kwenye mabonde yenye maji mengi ya—ya, au, kukaa katika mabonde yenye maji ya Sodoma na Gomora, na kuwa mchangamfu na kuishi kama wanawake wengine walivyoishi siku hizo.

64 Hakuchukua chaguo zuri, kama Sara ambaye alikaa katika nchi kame. Ila tu, aliweka Neno la Mungu moyoni mwake. Naye alikuwa mtiifu na wa kupendeza kwa mumewe, kiasi kwamba alimwita "bwana." Na hapo ndipo Mungu aliposhuka pamoja na Malaika wawili na kuwatembelea hemani.

65 Lakini, Bibi Lutu, alifanyika wa kilimwengu sana na kuchukuliwa na mambo ya ulimwengu. Basi hilo ni somo la jinsi gani kwetu, leo, kwamba tunaweza kuwa wenye nia ya kilimwengu kupita kiasi. Na nina hakika kabisa, leo hii, ya kwamba kanisa, kwa jumla, linakuwa na nia ya kilimwengu kupita kiasi. Sasa, labda, Bibi Lutu hakukusudia kufanya hivyo, aliposhuka kwenda kule. Aliwazia, "Nitakuwa tu mstaarabu." Ni sawa kuwa mstaarabu, lakini usizichukue tabia za ulimwengu.

66 Ukienda, nenda kama Shadraka, Meshaki, na Abednego, na Danieli. Waliazimu moyoni mwao kwamba hawatajitia najisi, hata iweje. Haidhuru kama kanisa lote lilirudi nyuma, kilichotukia, waliazimu moyoni mwao. Nao ni kumbukumbu leo.

67 Naye Bibi Lutu anasimama kama kumbukumbu. Ndipo wakati Mungu alipompa ujumbe wake wa mwisho wa neema, wakati alipowatuma hao Malaika kule chini na kuwaambia kwamba baada ya saa chache kwamba Sodoma na Gomora ingeteketezwa, hata hivyo, hangeweza kustahimili wazo la kuacha maisha yake ya kijamii, aingie jangwani, na kuishi kama Sara alivyokuwa ameishi kule jangwani, na kulazimika kuvaa nguo za kiraia, za kawaida za mwanamke wa kawaida. Alitaka kuwa katika anasa. Mumewe alikuwa amekuwa mtu mashuhuri mjini. Yeye aliketi langoni, kama hakimu au kama meya wa jiji. Naye alitaka anasa hizi. Wala asingeweza kuvumilia wazo la kuachana na mambo hayo. Naye alipokuwa akitoka nje ya mji, pamoja na mumewe, aliendelea kutazama nyuma, akilia na kuhuzunika kwa sababu ilimbidi ayaache, apate kujitenga na kifo cha namna hiyo.

68 Yesu alisema, "Mtu atiaye mkono wake kulima, kisha akageuka kuangalia nyuma, hafai kulima." Tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Mtu atiaye mkono wake kulima, na hata asi—asiangalie nyuma, lakini ageuke tu kuangalia nyuma, hafai hata kulima. Loo, tunapaswa kuweka macho na mioyo yetu pamoja. Haidhuru watu wengine wanafanya nini, yale kanisa lifanyayo, yale jirani afanyayo, yale mtu mwingine afanyayo, weka moyo wako umelenga Kalvari. Hata usisimame kuangalia nyuma. Hatuna wakati wa kuangalia nyuma.

69 Basi mwanamke huyu, kwa sababu alifanya hivyo, Mungu aliweka kumbukumbu kwa watu wote wanaogeuka kuangalia nyuma, wakiisha kumkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Aligeuka kuwa nguzo ya chumvi. Na amesimama pale hadi

wa leo, inaweza kuonekana makondeni, yule mwanamke anayesimama pale huku amekigeuza kichwa chake, akiangalia nyuma. Naye anatazama nyuma juu ya bega lake la kushoto, kutazama nyuma makondeni. Moyo wake ulikuwa huko nyuma. Hata hivyo, alilazimishwa, tuseme, kufanya hivi.

70 Na watu wengi humchukua Kristo hivyo, leo hii, kwa sababu wametoka ulimwenguni, wanajisikia kana kwamba wamelazimishwa kufanya hivyo. Na wanaendelea kuwa na shauku na kutamani, ndipo haichukui muda mrefu kabla hawajarudi nyuma. Nao—nao ni kumbukumbu ya kutisha ya neema ya Mungu, ya upendo wa Mungu kama vile ulivyoonyeshwa kwao. Sasa, kumbukumbu!

71 Sasa, katika siku za Yesu, akiwa duniani, Wayahudi walikuwa wamejenga hekalu kama kumbukumbu. Nao walikuwa wamemwonyesha Yesu jinsi hekalu hilo lilivyojengwa vizuri. Naye akasema . . . Ilichukua miaka arobaini kujenga hilo hekalu; kama miaka themanini, kwa jumla. Kwa miaka arobaini, walikuwa wakikata mawe katika sehemu mbalimbali za dunia. Miaka arobaini katika ujenzi wake, hakuna sauti ya msumeno wala sauti ya nyundo.

72 Lakini, mnajua, hata Yesu alisema hapo, "Msijisumbue kuliangalia hili, kwa maana nawaambia, ya kwamba utakuja wakati ambapo halitasalia jiwe moja juu ya jingine, jiwe moja juu ya jingine."

73 Hapo awali tu, Yeye alisema Maneno haya makuu ya kumbukumbu, "Mbingu na nchi zitapita, mahekalu yatapita, kumbukumbu zitapita, bali Neno Langu ndilo kumbukumbu ya milele."

74 Ile safina imeoza, miaka kadhaa iliyopita. Makaburi ya manabii yameporomoka. Na kumbukumbu zote mbalimbali zimeoza, kwa kipindi kirefu sana cha wakati, kimelifagilia mbali jiwe. Lakini Neno la Mungu linabaki vile vile, zuri milele na milele. Changamfu tu na mpya usiku wa leo, kwa waaminio wa siku hii, kama lilivyokuwa siku ambazo lilinenwa.

75 Si ajabu, Eliya, asubuhi ya leo, katika ninii yetu . . . ujumbe ambao ndugu yetu alitupa. Walipotaka kujenga shule kuu kwa ajili ya manabii, kama kumbukumbu, lakini Eliya akachagua jambo lililo bora zaidi, muujiza wa Mungu kuinua chombo kilichozama na kukifanya kielee juu ya maji. Lilikuwa ni Neno la Bwana.

76 Basi aliye bora zaidi ni yeye, usiku wa leo, atakayelipokea Neno la Bwana, moyoni mwake, kama kumbukumbu, kuliko wale ambao watajaribu kujenga kumbukumbu kuu.

77 Si muda mrefu uliopita, niliposikia, nilipokuwa huko Italia, nilisikia habari za Mussolini, na ile sanamu kubwa yenye urefu wa futi arobaini na kitu, aliyoijenga kama kumbukumbu ya riadha, kwa kuwa yeye alikuwa ni mwanariadha. Nami nilitaka

kuona kumbukumbu hiyo. Na, mnajua, ilikuwa imelipuliwa ikawa unga na mashine ya kubomoa.

78 Nilisimama, yapata miaka miwili, mitatu iliyopita, mahali ambapo mafarao wa Misri walikuwa wameinua madhabahu makubwa pamoja na sanamu. Nami. . . Wananiambia kwamba utalazimika kuchimba futi ishirini chini ya ardhi, kupata hata sakafu ambapo kumbukumbu hizo zilisimama.

79 Nilisimama mahali ambapo Kaisari Agusto, ambapo Maherode na watu mashuhuri wa Urumi. Nami nikaenda mtaani, na ambapo alikuwa akishuka mtaani kutoka kwenye ikulu, na ni kama futi ishirini na tano chini ya ardhi. Kumbukumbu hizo zimetoweka.

80 Lakini Neno hilo lililo hai la Mungu lingali lile lile na ni la thamani vile vile. Hiyo ni kumbukumbu.

81 Kwa hiyo nasema, leo hii, ndugu, mambo ufanyayo, maneno unayosema, jinsi unavyomtendea jirani yako, na kile unachofanya kuhusu Kristo, kitakuwa kumbukumbu ya kudumu. Unaweza kuwa na nyumba nzuri ya kuwaachia watoto wako. Unaweza kuwa unafanya kazi kuchuma riziki, kuwaachia watoto wako. Lakini afadhali niwaachie Neno la Mungu kuliko kitu kingine chochote. Nyumba hizo zitatoweka. Hiyo ni kweli kabisa, hilo ni zuri. Sina neno dhidi yake. Lakini usifanye mambo hayo madogo na kutoyafanya mambo makuu, unaona. Kwa sababu, Neno litaninii. . . Nyumba itaangamia, nao watu wataangamia pamoja nayo. Lakini Neno la Mungu litawafufua katika siku za mwisho, na kuwapa tena Uzima wa Milele usiopatikana na mauti. Na, sasa, ili kufanya milki kama hii, Neno la Milele la Mungu!

82 Ninauwazia wimbo huu wa kale tuliokuwa tukiimba hapa, miaka kadhaa iliyopita:

> Wakati umejaa mapito ya haraka,
> Hakuna kitu duniani ambacho hakitatikiswa,
> Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
>
> Safari yetu itakapomalizika,
> Iwapo tumekuwa waaminifu kwa Mungu,
> Nyumba yetu ya Utukufuni itakuwa nzuri na
>   angavu,
> Nafsi zetu zenye furaha tele zitaiona!

83 Ni bora zaidi jinsi gani kutazama nje, katika kutua kwa jua, wakati mishipa yako inapopoa mwilini mwako, wakati watoto wako wamesimama kukizunguka kitanda, kujua ya kwamba umejengewa kumbukumbu, kwamba, "Mpenzi, siku moja baba atakutana nawe ng'ambo ya pili!" Afadhali niwe na hiyo.

84 Daktari aliposema, "Billy, hakuna kingine unachoweza kufanyiwa."

85 Nami niwaone watoto wangu, na kuwaaga kwa busu. Niseme, "Lakini baba hafi. Anaenda kupumzika, Mahali fulani. 'Kwa maana nyumba hii ya maskani yetu iliyo ya duniani ikiharibiwa, ninayo inayongoja.'" Ni kumbukumbu ya jinsi gani kuzungumzia! Ni afadhali nifanye hivyo, mbele ya watoto wangu, kuliko kusema, "Mpenzi, nina dola milioni moja katika benki *hii*, na milioni moja hapa katika *hii*, kwa ajili yako." Afadhali niache ushuhuda huo.

Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
Anayesafiri juu ya bahari adhimu ya maisha,
Kwa ajili ya ndugu mpweke aliyepata ajali ya
meli baharini,
Akiona, atajipa moyo tena.

Kabisa! Waachie kumbukumbu, shuhuda zako.

86 Jinsi ninavyowazia, usiku wa leo, juu ya mzee mmoja aliyelala kule, katika saa zake za mwisho za maisha haya, walinipigia simu hivi majuzi na wananitaka nihubiri mazishini mwake; Maskani ya Paul Rader. Huyo ni rafiki yangu mwema, F. F. Bosworth, mtakatifu mtauwa anayeenda kumlaki Muumba wake. Naye akasema, "Huu ndio wakati wa furaha sana maishani mwangu, Ndugu Branham." Akasema, "Nina furaha sana kujua kwamba ninaenda kumlaki, ni vigumu kwangu kupata usingizi usiku."

87 Nimesikia habari za Bibi Aimee McPherson; si kumdharau, mwanamke wa ajabu. Naona alama katika *hili* na *lile*. Ninaona alama za Smith Wigglesworth na Dr. Price, na wengi wa watu hao wakuu, lakini hakuna hata alama moja niliyowahi kusikia mtu yeyote akisema kuhusu F. F. Bosworth. Mungu, mwisho wangu na uwe hivyo, kumbukumbu ya neema ya Bwana Yesu Kristo!

88 Nawazia juu ya E. Howard Cadle hapa juu, si muda mrefu uliopita, alipokuwa amelala sakafuni, kama mlevi sugu, huku n—nzi wakiruka kinywani mwake. Naye mama yake mkongwe mpendwa kule chini alikuwa ameomba na kuamini, na kumshikilia Mungu, kwa ajili ya mvulana wake mlevi. Hapo, alipouacha ulimwengu, aliacha ushuhuda na kumbukumbu ya neema ya Mwenyezi Mungu ambayo inatosha. Neno la Mungu linapowekwa Kwake, katika maombi, Mungu hana budi kujibia hilo.

89 Mungu analijenga Kanisa kama kumbukumbu, kumbukumbu ya dhabihu Yake. Kristo hakuja duniani kufa bure. Kifo chake hakitakuwa bure. "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Ikiwa watu hawataliishia, kama hawatalichukua na, kulizingatia, na kutambua ni zawadi kubwa jinsi gani ambayo Mungu amewapa,

Mungu anaweza kutoka kwa haya mawe kumwinulia Ibrahimu watoto. Kweli atawainua! Nami ninapowazia hilo, na kuwazia juu ya gharama kubwa iliyompasa kulipa! Sasa ni vema . . .

90 Kila mtu anataka kila kitu bure, anataka kila . . . Hiyo ndiyo njia ya maisha ya Marekani siku hizi. Kupata kila kitu unachoweza bure. Ndugu, hupati kitu chenye thamani yoyote, bure. Unalipia unachopata. Hiyo ni kweli. Huna budi kukilipia, nacho kina gharama kubwa.

91 Nao wokovu wako ulikuwa na gharama kubwa, kwa Mungu. Unagharimu Mwanawe wa pekee, kumpa kila mtu Uzima wa Milele na kumfanya kuwa na furaha, usiku wa leo, na kuyaishia mambo ambayo yanafaa kuishiwa. Sio kuwaachia kitu watoto wetu; hakuna urithi utakaoachwa, mkuu kuliko wokovu wa Bwana wetu Yesu. Hakika, sivyo.

92 Sasa, gharama kubwa zinalipwa. Jaribio la wakati halina budi kufanyika. Ni kumbukumbu zilizojaribiwa na wakati. Nayo kumbukumbu ya pekee iliyowahi kujaribiwa vyema, imekuwa ni Neno la Mungu. Loo, makafiri wamejaribu kulizima. Wamefanya kila waliloweza kufanya, lakini halitapita kamwe. Haliwezi kushindwa kamwe.

93 Ibrahimu, wakati alipopokea kumbukumbu hiyo ya Mungu, "Utapata mtoto kwa mwanamke huyo, Sara." Miaka ishirini na mitano, aliliamini kwa moyo wake wote, na kukana chochote kinyume chake, kwa maana alijua ya kwamba Mungu angetimiza Neno Lake.

94 Makafiri, siku hizi, wanainuka na kujaribu kuipaka matope Biblia. Kabla hujaweza kuikomesha Biblia, ingekulazimu kuusimamisha wakati kabla hujaweza kufanya hivyo. Kila ulimwengu mkanamungu, kila watu wakanamungu, kila watu wa kikomunisti, na chochote walicho, kila mfuasi wa Budha, kila Mjaini, kila Mwislamu, hana budi kushuhudia kuzaliwa kwa Bwana Yesu Kristo, kila siku. Vema, kila unapotia sahihi barua, amina, kila unapoandika tarehe, unashuhudia kwamba Mungu alimtuma Mwanawe, miaka elfu moja mia tisa na hamsini na saba iliyopita. Ndugu, hungeweza kufanya hivyo. Kamwe isingewezekana. "Mbingu na nchi zitapita, lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe."

95 Wakati fulani uliopita, nilikuwa New York, nikaenda kwenye kisiwa kidogo, kwenye ile Sanamu ya Uhuru ambayo ilipewa . . . iliyopewa Marekani na serikali ya Ufaransa, miaka mingi iliyopita. Na mkononi kuna nuru ya tochi. Tulipanda hadi kwenye mkono huo. Kuna dirisha hapo. Na ambapo nuru hii kuu ilikuwa ikimulika, niliona kote kando kando yake kulikuwa na kundi la maskini shomoro, nao wote walikuwa wamekufa, wamelala kando. Nami nikamwambia huyo kiongozi, "Vipi shomoro wale? Je, walikufa kwa umeme?"

96 Kasema, "Hapana, bwana. Hatujawaokota bado asubuhi ya leo." Kasema, "Jana usiku kulikuwa na dhoruba, dhoruba kubwa ilipitia kwenye hili ghuba hapa."

Nikasema, "Naam, bwana. Ninajua hilo."

97 Akasema, "Maskini hao jamaa walinaswa katika hiyo dhoruba." Kisha kasema, "Walipoingia kwenye nuru hii, walijaribu kuizima hiyo nuru. Mnaona? Waligonga tu na kukigonga hiki kioo." Kisha kasema, "Badala ya kuitumia nuru waende mahali pa usalama, walijaribu kuizima hiyo nuru."

98 Ndipo uvuvio ukanijia. Hiyo ni kweli. Wanaume na wanawake ambao wanajaribu kuizima Nuru ya Mungu, wanaponda-ponda tu akili zao. Basi, hiyo Nuru, kwa nini wasiitumie kwenda kwenye usalama, badala ya kuponda-ponda akili zenu? Wanajaribu na kuikana, na kusema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, hakuna wokovu wa moyoni, mambo haya." Wanagonga-gonga tu nguzo. Mradi wanafanya hivyo, Kanisa kuu la Mungu linasonga mbele na kwenda juu, haraka tu liwezavyo kwenda. Watu wanainuka na kudai kuwa ni *hiki*, na *kile*, na kushindwa, na kadhalika. Lakini Kanisa la Mungu linasonga mbele, nalo Neno la Mungu linaendelea mbele. Limetengenezwa kwa nyenzo sahihi.

99 Si muda mrefu uliopita, kule chini Australia, ile Australia kuu iliyo chini ya utawala wa Uingereza, ni kama Afrika Kusini, ng'ambo tu kuelekea Australia. Huko chini Sydney, kuna mji mkubwa unaoizunguka ghuba kule, Ndugu Beeler labda anajua zaidi kuuhusu kuliko vile ningejua. Hata hivyo, walitaka kujenga daraja, kuvuka kutoka—kutoka Sydney Kaskazini hadi Sydney Kusini. Waliitana kote nchini, kupata wasanifu majengo, wajenzi wa madaraja, washuke waje wakajenge daraja hili. Hakuna hata mmoja wao angeweza kuichukua. Hakuna aliyethubutu kuichukua. Mara walipofika huko, waligundua kwamba chini ya bahari hii ni mchanga unaodidimia. Ulikuwa ni mchanga didimizi, wala hakuna kitu kingeweza kusimama. Nao wakaupima na kuuvumisha, na kuendelea. Wakasema, "Hapana, hata tusingeanza kujaribu kujenga daraja kama hilo. Haiwezekani."

100 Baada ya kitambo kidogo, msanifu majengo mchanga kutoka huko Uingereza akaja, mtu maarufu, mtu mwenye sifa nzuri, alikuwa na sifa nzuri.

101 Loo, napenda hilo! Napenda mtu mwenye sifa. Loo, si lazima uwe mtu mkubwa. Unaweza kuwa ombaomba anayeishi vichochoroni, na kuwa na sifa bora zaidi kuliko mtawala. Kabisa. Si lazima uwe tajiri. Unaweza tu kuwa na sifa. Inatangaza, sifa zako na kile ulicho, inakufanya kile ulicho. Inakupa sifa zako. Nawe unajulikana kwa sifa zako.

102 Mtu huyu alishuka huko akiwa na sifa njema sana. Akaangalia hali ya mambo. Akatembea ufukoni kwa siku

chache. Akauchunguza. Akaupima. Akauvumisha. Akaangalia pande zote. Baada ya kitambo, akamwendea meya, akasema, "Nitaichukua hiyo kazi."

"Mbona," akasema, "bwana, unajua unachochukua?"

Akasema, "Ninaelewa kabisa."

103 Akasema, "Vema, msanifu majengo huyu mkuu asema . . . Wasanifu majengo wa Marekani na wasanifu majengo kutoka kote ulimwenguni, wajenzi wa madaraja, wamekuja hapa, na wanaiogopa hii kazi."

104 Akasema, "Lakini, bwana, mimi siogopi kazi hii. Nitaichukua." Akasema, "Ninatambua kwamba nina sifa duniani kote, kama mjenzi wa daraja; lakini nitaweka hatarini sifa zangu, kwa maana ninaweza kuijenga." Loo, alikuwa na ono! Kabla ya mtu kupata sifa, hana budi kuwa na ono la kile anachofanya.

105 Loo, Bwana na abarikiwe! Hiyo ndiyo sababu kuna Mbingu ya kuendea. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kuwa na sifa kama Mkristo, tunajua ni nyenzo gani zilizo katika jengo hili. Hiyo ni kweli. Ni Damu ya Yesu Kristo iliyo katika jengo hili. Hiyo ni kweli. Damu Yake iliyotiwa doa imeosha na kuondolea mbali dhambi zote. Alinitoa kwenye vichochoro vya kuzimu na kunifanya mtumishi Wake. Basi, ninamwamini Yeye. Kwa hiyo, nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Na kila muumini amefanya hivyo, kwa sababu wana imani na wanamwamini Mjenzi huyu mkuu, na Msanifu majengo huyu mkuu.

106 Sasa, mtu huyo alipofanya hivyo, jambo la kwanza alilofanya, kuhakikisha kwamba alikuwa sahihi, alienda kule chini. Naye akasema, "Sasa, kabla hatujaanza kujenga daraja hili, hatuna budi kwenda kwenye msingi imara. Hatuna budi kwenda." Alijua ya kwamba chini ya mchanga huo, kifua cha dunia kilikuwa pale, ambacho kilikuwa ni mwamba mtupu. Alifanya nini ila kuchukua pampu kubwa mno? Ndipo akaingia mle ndani na kuweka mabomba makubwa chini, kisha akapuliza mchanga didimizi, kwa pampu hizi, mpaka akaupeperushia mbali akafikia kwenye mwamba imara. Alipofika mwambani, alifungia hizi bolti kubwa sana mle ndani, na kuzifanya tayari. Naye akapulizia kila moja.

107 Kisha akaenda huko akawaleta, karibu naye, wasanifu majengo bora sana ambao angeweza kupata, wanasayansi bora zaidi, vifaa bora zaidi. Akaagizia na kuletewa feleji kwa ajili ya daraja lake. Alipofanya hivyo, asingeweka kipande kimoja cha feleji, si hata bolti moja, mpaka ilipojaribiwa kisayansi; aone kama kulikuwa na mianya yoyote ndani yake, kuona kama kulikuwa na mashimo yoyote madogo ya hewa ambapo, kwenye kiwanda cha chuma, ambapo waliitengeneza na kuifinyanga, aone kama imefanyiwa uchunguzi sawasawa.

Loo, hiyo ingekuwa ni ku—kumbukumbu ya jinsi gani, iwapo . . . kwa sifa zake kama mjenzi wa daraja.

108 Kama alisumbuka hivi, ili kuhakikisha kuwa hilo daraja litakuwa salama, mnafikiri Mungu alisumbuka kiasi gani, kuhakikisha Kanisa hili lingekuwa salama? Naam, bwana. Kuna kumbukumbu ya kifo cha Kristo, hiyo ni Kanisa Lake. Watu wengine hawataki kuiishi, watu wengine wataiishi. Lakini, ni wakati wa kujaribiwa. Mungu anawajaribu watu, leo hii, kwa ajili ya kumbukumbu Zake.

Mara nyingi, watu husema, "Loo, ninajaribiwa sana!"

109 Jina la Bwana libarikiwe, kwa ajili ya majaribu! "Ninapokuwa dhaifu, basi nina nguvu," Alisema Paulo. "Kila mwana amjiaye Mungu, hana budi kwanza kujaribiwa na kupimwa." Nayo majaribu haya ni matamu zaidi kwako, na yanapendeza zaidi kwako, kuliko dhahabu ya thamani. Ni wakati wa kujaribiwa.

110 Zamani za kale, kabla hawajawa na viyeyushaji, walikuwa wakichukua dhahabu . . . Na jinsi wangejua kama ilikuwa ni nzuri au la, na uchafu wote umetoka ndani yake, uchafu wote wa chuma (hiyo ni dhahabu ya mpumbavu), upumbavu wote umetoka ndani yake, wao . . . Wapigaji waliipiga, na kuipiga na kuigeuza, na kuipiga na kuigeuza, mpaka mpigaji akaona uakisi wake—wake katika hiyo dhahabu.

111 Hivyo ndivyo Mungu anavyolitendea Kanisa Lake. Anakupa jaribu baada ya jaribu, mtihani baada ya mtihani, jaribu baada ya jaribu, kipimo baada ya kipimo, mpaka Uzima wa Kristo uonekane katika maisha yako; mpaka unakuwa na amani, kiasi, upole, utulivu, unyenyekevu, tayari, mtiifu, aliye tayari, unageuza kichwa chako kutoka kwenye mambo ya ulimwengu, na kuangalia moja kwa moja kuelekea Kalvari, kwake Yeye Yule ambaye anapiga. Mara nyingi unafikiri ni ajabu kwa sababu ya majaribu motomoto, magonjwa, na mateso. Yanafanywa tu ili kukujaribu, kukuondolea uchafu, kukuondolea tope, kukuondolea uzembe, kukuamsha hadi mahali ambapo unaweza kutazama na kuona ule uakisi, au mtu anaweza kuona uakisi wa Kristo ndani yako, "Kristo ndani yako, tumaini la Utukufu."

112 Alijaribu kila kipande. Hatimaye, yeye . . . Kabla ya kutia bolti, aliijaribu. Alijaribu kila kitu.

113 Ndipo alipomaliza yote, sasa, wale wenye kudhihaki walisimama karibu na kusema, "Haitashikilia. Haiwezi kushikilia."

114 Hivyo ndivyo wanavyosema leo. "Dini hii hapa ya Roho Mtakatifu mnayozungumzia, haitachukua muda mrefu, mti huo utateketea." Lakini hauteketei.

115 Loo, mo—moto huumwagilia tu maji. Unatupatia tu tumaini jipya. Una—unauimarisha tu; kila jaribu, kupimwa. Kila wakati

upepo unapoupiga mti na kuusukuma mbele nyuma, na huku na huku, hulegeza tu mizizi ipate kuingia ndani zaidi na kushikilia vyema. Kila mara ugonjwa unapoikumba nyumba yako, kila wakati jaribu linapoikumba nyumba yako, kila wakati majirani wanaposema jambo baya juu yako, inakutikisa tu, kukulegeza, ili uweze kushuka na kuushika vyema Mwamba wa Milele wa Neno la Mungu lisilotikisika. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Anatuma majaribu hayo apate kukujaribu na kukuhakikisha, kukutikisa na kukupa mshiko mpya.

116 Ndipo tunaona, alipomaliza hayo yote, wakosoaji walisimama karibu na kusema, "Haiwezekani." Lakini nini? Msanifu majengo alijua daraja lake lingeshikilia. Alijua lingeshikilia, kwa maana lilikuwa limejaribiwa.

117 Hiyo ndiyo sababu Mungu alisema, "Nitakuwa na Kanisa lisilo na ila wala kunyanzi." Amina. Alikuwa amepita majaribuni. Na kila mtoto amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa.

118 Katika siku ile kuu ya ukumbusho, walipokuwa wakienda, pande hizo mbili zilipoanzishwa kutoka pande zote mbili, walipokutana katikati ya hilo ghuba, yule mtu aliyekuwa amelijenga, alisema, "Sitamwomba mtu yeyote."

119 Wasanifu majengo wote waliosimama pande zote, wakasema, "Mara mtetemo wowote utakapoligonga daraja hilo, litaporomoka moja kwa moja. Litakuwa hatari." Hakuna kampuni ya bima ingempa bima juu yake.

120 Hakuhitaji bima yoyote. Alisema, "Daraja langu litashikilia." Alikuwa na imani. Sasa, lazima alijaribu, kwa sababu sifa zake ziko hatarini. Bila shaka, ziko hatarini. Na kama lisingestahimili, lingekuwa ni kumbukumbu.

121 Hiyo ndiyo sababu ninajua ya kwamba wokovu wa mtindo wa kale, wa moyoni, wa Mungu, utashikilia: sifa za Kristo ziko kwake. Yeye hatatupa kitu cha kujengea Kanisa, si theolojia ya kujibunia, si juu ya uzoefu fulani wa shule, ama kujenga seminari kama walivyotaka, asubuhi ya leo, kuwaelimisha wahubiri. Mhubiri halisi anatoka katika seminari ya neema ya Mungu, wito wa Mungu, nao umejaribiwa na wakati. Hiyo ni kweli. Utashikilia. Mungu ana imani nawe. Tuna imani Naye. Daraja litaninii . . . Mshairi wa kale alisema:

> Nanga yangu inashikilia ndani ya pazia;
> Katika kila upepo mkali wa dhoruba,
> Nanga yangu inashikilia ndani ya pazia.

122 Hatujui kinachoshikilia, lakini Kitu fulani kinashikilia. Hiyo ni kweli. Imetiwa nanga kule kwenye kimbilio. Na kuna kamba ya wokovu ambayo inaushikilia moyo wa mwanadamu, ambayo mtu ambaye amewahi kuzaliwa mara ya pili amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Pepo wote kutoka kuzimu wasingeweza kumfanya atilie shaka. Kuna Kitu

fulani kinachoshikilia mle ndani. Acha ayumbeyumbe! Acha atikisike! Amina. Atashikilia, kila wakati, kwa sababu yuko katika Kristo Yesu.

123 Basi mtu huyu akasema, "Sitamwomba mtu yeyote, lakini," kasema, "Nitaenda, mimi mwenyewe."

124 Meya wa jiji akatoka nje na kusema, "Bwana, hakika nina imani na daraja lako."

125 Akasema, "Ikiwa una imani na daraja langu, nifuate. Vema, tulijaribu."

126 Meya akasema, "Gari langu litakuwa limesimama pale asubuhi fulani hiyo. Nitakwenda pamoja nawe."

127 Shirika la reli likapiga simu na kusema, likapiga simu na kusema, "Bwana, tuna imani na daraja lako. Tutakuwa na . . . "

128 Kasema, "Ikiwa mna imani na daraja langu, leteni magarimoshi manne yaliyojaa mizigo, myaweke kwenye daraja. Ikiwa mna imani, nifuateni. Ikiwa mnaamini kuwa limepimwa na limejaribiwa, mnaliamini, njoni, mwambatane nami."

129 Na wengi wa watu walimwandikia barua, kuona ujasiri wake. Hicho ndicho watu wanachoangalia ni watu wenye ujasiri, si kitu kisicho na msimamo.

130 Ikiwa unafikiri unaweza kukwepa, kwa kwenda kanisani na kusema "amina" mara moja moja, na kupaza sauti kidogo, kuweka jina lako kwenye kitabu, na kurudi na kuishi kama ibilisi, matendo yako mwenyewe yanathibitisha kile ulicho. Tabia yako imelithibitisha. Lakini Mungu . . .

131 Ulimwengu unataka kuona watu ambao ni jasiri, mtu mwenye ujasiri, ambaye atajitokeza, kama kumbukumbu ya neema iokoayo ya Yesu Kristo. Hiyo ni kweli.

132 Ile siku ambayo lile daraja lilipoanza, hao wengine walirudi, wakasema, "Iweni tayari. Tayarisheni kamera zenu," hao wote, waandishi wa habari walisema, "kwa sababu daraja lile litaporomoka."

133 Jamaa huyo mchanga alitembea kule nje kwenye daraja hilo, akaliweka gari lake chini, akatazama nyuma, akaona hayo magarimoshi yote yamepanga msafara, akamwona meya pale akimpungia mkono. Akatazama akaona makumi ya maelfu ya watembea kwa miguu wamesimama hapo nyuma, tayari kuandamana naye. Kasema, "Cheza bendi." Ndugu, bendi zilipoanza kucheza, filimbi zikaanza kulia, baragumu zikaanza kulia, ninamaanisha kulikuwa na mtetemo mbaya sana uliokuwa ukifanyika. Lakini yeye akavuka moja kwa moja kwenye daraja hilo, wala kamwe halikutikisika. Kwa nini? Alichukua nafasi ya mbele, maana, kama lingeanguka, acha aangamie pamoja nalo.

134 Naye Yesu Kristo alikuja kutoka Mbinguni, Utukufuni; kutoka Utukufuni, akashuka huku, kujenga Kanisa. Na nyenzo ambazo Yeye anaweka ndani Yake, ni nyenzo zilizojaribiwa na wakati. Unaweza kuja madhabahuni na kufanya maungamo, lakini Yeye anapopata mashimo yaliyotobolewa na hewa na kadhalika, unaona, ulimwengu—ulimwengu umekupulizia na kuingiza funza ndani yako, na kadhalika, huwezi kusimama. Anakusukuma tu upande mmoja. Mungu anataka Kanisa lililojaribiwa na wakati; si mtu ambaye ni Mkristo leo na kesho amerudi nyuma, kuingia na kutoka, na huku na huko. Hawezi kukuweka popote.

135 Bali ana Kanisa lililojaribiwa, likapitia majaribuni, katika hasara, katika maradhi, katika huzuni, katika kifo, na bado linasimama na ushuhuda. Huyo ndiye mtu, naam, huyo ndiye mtu Yeye anamtafuta. Sijali kama wewe ni ombaomba. Sijali kama wewe ni mwombaji. Sijali kama wewe ni mwokota-matambara. Chochote ulicho, Mungu anakuwekea jaribio. Anatafuta nyenzo zilizojaribiwa na wakati. Ninaamini, moja ya siku hizi wakati Kanisa hilo kuu . . .

136 Wakati, sayansi inaposema, "Inawezaje kuachilia? Nguvu za uvutano zinakushikilia duniani."

137 Sasa ninajisikia kubarikiwa. Hebu niwaambie. Kanisa hilo lililojaribiwa na wakati litakuwepo siku moja. Huenda ikawa nusu yao wamelala katika mavumbi ya ardhi. Sijui walipo, lakini Mungu amezijaribu nyenzo Zake zote. Siku moja Yeye anakuja kuchukua mstari wa mbele: "Nifuateni!" Moja kwa moja kupitia angahewa na anga za juu, na nyanja na nyanja, hadi kwenye Uwepo wa Mwenyezi Mungu atakwenda, pamoja na Kanisa lililojaribiwa na wakati. Hiyo ni kumbukumbu ya neema Yake; hiyo ni kumbukumbu ambayo Mungu anampa.

138 "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Na kila mtu amjiaye Kristo ni zawadi ya upendo kutoka kwa Mungu, naye Kristo humtia majaribuni. Na kama akistahimili majaribu, anamweka kwenye daraja, anamkaza, anampa nafasi, na kumweka pale, akijua ya kwamba atashikilia hata mwisho wa safari. Amina. Nyenzo iliyojaribiwa na wakati!

139 "Juu ya Mwamba huu," si juu ya mwamba fulani wa ulokole, si juu ya lundo la mihemuko, si juu ya lundo la theolojia ya kanisa, si juu ya madhehebu fulani. Lakini, "Juu ya Mwamba huu imara," Neno la Kristo, "nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kamwe kulishinda." Litakuwako.

140 Itakuwa kumbukumbu ya neema Yake, mbele za Malaika. Malaika walipomwuliza swali, siku moja, "Kwa nini unakwenda duniani?" Atarudi na kuliwasilisha Kanisa hilo bila hatia, bila ila, bila kunyanzi. Hizo hapo nyenzo. Jambo ndilo hilo. Sifa zake. Inambidi kufanya hivyo. Mjenzi huyo wa daraja ilimbidi kulijenga hilo daraja; hana budi kulijenga, la sivyo apoteze

sifa zake. Kristo atakuwa na Kanisa, naye hana budi kufanya hivyo. Kwa sababu, Yeye alikuja duniani na kufanyika mwili, na kukaa miongoni mwetu; kisha akafanyika dhambi, ili tupate kuwa wenye haki. Yeye alifanyika sisi, kusudi sisi, kwa neema Yake, tuweze kuwa Yeye. Alikuja kupachukua mahali petu, kama mwenye dhambi; kuturuhusu kupachukua mahali Pake, kama wana na binti za Mungu, katika Uwepo wa Utukufu Wake. Ni neema iliyoje ya Mungu!

141 Tungewezaje kusema, "Hayo Maneno si sahihi"? Mbingu na nchi zitapita, lakini Maneno hayo hayatapita kamwe.

142 Mvulana mdogo kipofu wa Kihindi, siku chache zilizopita usiku, kipofu tangu alipokuwa na umri wa majuma matatu—matatu ama manne, alifumbuliwa macho, kama kawaida, na akatoka jukwaani akitembea. Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni kumbukumbu ya Nguvu na neema za Yesu Kristo iliyojaribiwa na wakati. Jina Lake takatifu lihimidiwe!

143 Kujaribiwa na wakati! Majaribu, shida, mtikisiko, na kuvuta, ni kupata tu mianya ndani yako, kuona kama kuna wowote humo. Ni Mungu anayekutikisa na kukujaribu.

144 Siku moja, Kaisari Agusto mkuu, baada ya vita vikuu maarufu, na akiisha kupata ushindi mkuu, yeye. . . walikuwa wanaenda kumfanyia sherehe huko Rumi. Naye akawaambia, "Ninataka mtu fulani apande, mtu mstahilifu, apande kando yangu ninapofanya hivi." Kasema, "Nataka mtu wa kushiriki baraka hizi pamoja nami." Basi wote. . . Ilitangazwa kwenye kambi zote. Maafisa wote wakachonga manyoya yao, na kung'arisha mapanga yao, na kuzing'arisha sana silaha zao, na kila kitu, kisha wakajizoeza kusimama wima, na saluti fulani kwa mfalme wao, na kadhalika.

145 Na kila mmoja akapanda, silaha zao kubwa mbele yake, alipokuwa ameketi pale kwenye kiti chake cha enzi, akitazama. Ndipo akaja, ofisa pamoja na manyoya yake makubwa, mazuri, makali tu, akasimama na kupiga saluti yake. Kaisari akatikisa kichwa; huyo akaenda zake. Mwingine akatokea, akapiga saluti yake. Kaisari akatikisa kichwa chake; naye akaenda zake. Muda baada ya muda, askari baada ya askari.

146 Hatimaye, chini kabisa mstarini, akaja maskini mtu wa miguu. Hakuwa na ngao yoyote ya kung'arisha, wala hakuwa na unyoya wa kuchonga. Lakini akatembea mbele ya Kaisari. Hata hakujua jinsi ya kupiga saluti ifaayo, lakini aliinamisha tu kichwa chake na kuondoka.

147 Kaisari akasema, "Hebu kidogo. U nani wewe? Rudi hapa." Akarudi pale. Akamtazama. Kuna makovu usoni mwake, na amekatwa, na kuharibika sura, na ni kilema. Kasema, "Kwani ulipata wapi makovu hayo?"

Akasema, "Huko nje vitani, nikimpigania bwana wangu, Kaisari."

148 Akasema, “Panda hapa ukaketi karibu nami. Wewe ndiwe umejaribiwa na kuthibitishwa.”

149 Ndugu, si wakati wa kuchonga manyoya, si siku za kielimu. Ni wakati wa kujaribiwa na wakati. Ni wakati ambapo Mungu analijaribu Kanisa Lake kuona makovu ya vita vya majaribu makali, na mapigano, na vita. Huyo ndiye atakayepanda kando Yake.

150 Jinsi Elisha alivyoaribiwa na kuthibitishwa, kabla hajavaa joho la nabii! Jinsi Elisha alivyorusha joho hilo begani mwake! Jinsi hana budi kuwa mtu anayefaa! Elisha alimtazama pale shambani, alipokuwa akilima. Mungu akasema, “Huyo ndiye yule mtu. Huyo ndiye mtu anayeweza kuvaa vazi hilo. Huyo ndiye mtu anayeweza kuvaa joho hilo. Anaweza kupachukua mahali pako.”

151 Jina la Bwana libarikiwe! Jinsi ambavyo jicho lake linaloona kila kitu linavyotembea juu ya nchi, akijaribu kumtafuta mtu ambaye atavaa joho hilo ambalo alinena habari zake. “Mnaweza kunywea kikombe ninyweacho Mimi? Je, mnaweza kubatizwa kwa ubatizo nibatizwao Mimi? Mnaweza,” Alisema hivyo.

152 Kwa hiyo, sisi, leo hii, kama Kanisa, mnapaswa kuvaa joho la Kristo; silaha zote za Kristo, ngao yote na kikingio, na silaha, tupate kusimama bila lawama Siku ile. Anatafuta kumbukumbu zilizojaribiwa na wakati, ambapo anaweza kusema, “Yule pale mtumishi Wangu. Nimempima. Nimemjaribu. Nimempitisha, kama Ayubu. Angali anathibitisha asilimia mia moja.” Mungu na aturehemu, hata tuweze kuliamini Neno Lake Mungu, na kuwa kumbukumbu zilizojaribiwa na wakati.

Na tuombe.

153 Baba mbarikiwa, tunakushukuru Wewe, Mungu Mtakatifu Sana, kutoka kwenye vilindi vya mioyo yetu, kwa ajili ya kujaribiwa na wakati, kila majaribu. Hatujisikii vibaya juu yao, Bwana, lakini tunashukuru kwamba neema Yako ilitosha kutusaidia katika nyakati hizi kuu za majaribu.

154 Kama mtu yule, usiku wa leo, jinsi ilivyolisisimua kusanyiko, alipotaja, *Neema Ya Ajabu,* na tulipokifikia hicho kifungu fulani!

> Kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,
> Nimekuja tayari;
> Neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,
> Neema ndiyo itakayonipeleka mbele.

155 Loo, ilisisimua moyo wa watu! Tunaamini ilikuwa inaambatana na Ujumbe usiku wa leo, ya kwamba ilikuwa ni kujaribiwa na wakati, kupitia hatari, taabu na mitego. Ilikuwa ni kumsaidia Mkristo, yule ambaye amejichunguza mwenyewe sasa na kujua kwamba amesimama mwaminifu, kwa neema ya Mungu. Ilikuwa ni kuwaletea aibu wale walio na mianguko,

na mema na mabaya, wala hawajali, na maisha mabaya. Ee Mungu, hakuna hata kovu la vita la kuonyesha vita. Tunaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba utalitakasa Kanisa, kwa Damu Yako kuu takatifu, na kuyasafisha mapigo yote, na sehemu zote dhaifu, na—na nyuzi zote chafu. Wapitishe kwenye mtambo tena, na—na kuwagusa tena, Bwana, na—na kuwafanya nyenzo. Ee Baba wa Milele na mbarikiwa, yasikie maombi ya mtumishi Wako.

Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu.

156 Kama kungekuwako na mtu kama huyo hapa usiku wa leo, ambaye angejisikia ya kwamba Mungu, katika nyakati hizi za majaribu, hajawahi kukuona mwaminifu kazini. Wakati mabishano yanapoibuka, au unaruka ndani moja kwa moja na kuyashiriki? Ugomvi unapotokea, wakati kutojali, wakati tofauti kanisani zinapotokea, je, unaungana na dini potovu na magenge, na kadhalika namna hiyo? Je, unasikiliza umbeya mitaani na katika ujirani? Kama una hatia ya jambo hilo, umepuliziwa na mipulizo ya ibilisi, hebu turudi kwenye tanuru, usiku wa leo, na kuyeyushwa tena, na kutokea bila wao ndani yetu. Hebu Mungu atutie hesi na atuweke tayari kwa ajili ya Daraja kuingia katika Unyakuo Wake. Ikiwa mtu kama huyo yuko hapa, naye angetaka kukumbukwa!

157 Unasema, "Ndugu Branham, ninawezaje kujua ya kwamba kumbukumbu hii isiyopatikana na mauti, ya Milele itasimama?"

158 Nitakunukulia Neno Lake, kulingana na Yohana 5:24. "Yeye alisikiaye Neno Langu." (Si "Anayehudhuria shule Yangu.") "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

159 Je, unaweza kusikia Neno Lake likikuita, usiku wa leo? Kama unaweza, na ungetaka kukumbukwa katika maombi, naomba uinue mkono wako. Useme, "Ndugu Branham, niombee tu. Ninataka kuwa nyenzo ifaayo, ndipo Kristo atakapolitoa nje Kanisa Lake, kwamba sitakuwa . . . " Mungu akubariki, bwana. "Halitanitetemesha, Yeye ataniweka moja kwa moja Kanisani." Mungu akubariki, kijana mwanamume. Mungu akubariki, dada. "Ninataka kuwa . . . " Mungu akubariki, ndugu. "Ninataka kuwa nyenzo ifaayo." Mungu akubariki, ewe mtoto huko nyuma. Mungu akubariki hapa, ndugu yangu mpendwa. "Ninataka kupatikana kama nyenzo halisi. Nataka niweze kutoa ushuhuda wa tumaini lililo ndani yangu; tumaini!" Mungu akubariki, dada. Hilo ni jema. Hiyo ni sawa.

"Inafanya nini, Ndugu Branham, kwa kuinua mikono yangu?"

160 Unapita kutoka mautini kuingia Uzimani. Hivyo ndivyo unavyofanya. Unavunja kila kanuni ya nguvu za uvutano, papo hapo. Unaona, kama ungekuwa tu umbo la nta umeketi pale,

usingeweza kamwe kuinua mkono wako. Usingeweza kufanya hivyo. Lakini inaonyesha kuna roho ndani yako, roho, na roho hiyo imemsikia Roho wa Mungu akizungumza nawe. Na roho hiyo iliyo ndani yako imefanya uamuzi, kwa hiyo inapinga sayansi. Inaziasi nguvu za uvutano. Inatokea, inaonyesha kuna roho ndani yako, inayoweza kuuinua mkono wako. Kama ungalikuwa maiti, usingeweza kufanya hivyo, bali umekuja kwenye Uzima. Jambo fulani limetukia.

161 Ikiwa umekufa katika dhambi na makosa, Mungu hawezi kusema nawe tena, mkono wako utabaki chini. Kama hujafa katika dhambi na makosa, na Mungu anaweza kusema nawe, nawe ukapokea Uzima, utainua mkono wako. Unaona, inaonyesha Uzima umefanya uamuzi, umemkubali Kristo. "Umepita kutoka mautini kuingia Uzimani," kama unalimaanisha.

162 Limaanishe sasa, unapoinua mkono wako. Sema, "Mungu, unirehemu, unifanye ninachopaswa kuwa. Nami nitakutumikia Wewe maishani mwangu mwote. Nataka nipatikane tayari siku hiyo." Baraka juu yako, ndugu yangu mpendwa huko nyuma. Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo. Mungu akubariki, pale ndu-. . .Mungu awe nawe. Mungu akubariki, kipenzi. Vema, mtu mwingine. Mungu akubariki hapa, Ndugu Roy, na Bwana awe pamoja nawe. Naam. "Bwana, nipate mstahilifu. Nipate mstahilifu." Mungu akubariki, ndugu yangu huko nyuma kabisa. Bila shaka, Mungu anakuona. Furahini. Je, kuna mtu mwingine anayetaka kukumbukwa katika maombi sasa hivi? "Nifanye . . . " Vema. Hebu . . .

Kumbukumbu Za Mungu Zilizojaribiwa Na Wakati SWA57-0818
(Time-Tested Memorials Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 18 Agosti, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org